



(University of Choice)

MASINDE MULIRO UNIVERSITY OF SCIENCE AND TECHNOLOGY
SCHOOL OF ARTS AND SOCIAL SCIENCES
(MMUST)

UNIVERSITY EXAMINATIONS
2021/2022 ACADEMIC YEAR
THIRD YEAR YEAR SECOND SEMESTER EXAMINATIONS
SUPPLEMENTARY/SPECIAL EXAMINATIONS
FOR THE DEGREE OF
BACHELOR OF EDUCATION (ARTS)

COURSE CODE: KIS 303

COURSE TITLE: KISWAHILI POETRY

DATE:

04/08/2022

TIME

10 - 12 PM

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

JIBU MASWALI MATATU. SWALI LA KWANZA NI LA LAZIMA

TIME: MASAA MAWILI

MMUST HAIRUHUSU UDANGANYIFU WOWOTE KATIKA MTIHANI

This Paper Consists of 2 Printed Pages. Please Turn Over.

1.a. fafanua dhana ya ushairi. (alama 4)

b. kwa kutolea mifano jadili sabaabu zozote nne za mgogore katika ushairi wa Kiswahili. (alama 16)

1. a. Jadili jinsi ambavyo maudhui yafuatayo yanavyodhihirika katika utenzi wa Fumo Liyongo.

i. Ushujaa wa Kiafrika

ii. Tamaa na ubinafsi (alama 20)

2. "Subira ni jambo la muhimu maishani". Tetea ukweli wa kauli hii kwa kurejelea mashairi manne kutoka katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* (s. *Abdala*) (alama 20)

3. Jadili maudhui yoyote manne kutoka mojawapo wa diwani zifuatazo

a. *Mchezo wa Karata* – kitheka Wamberia

b. *Chembe cha Moyo* - Al Amin Mazrui

4. Kwa kutumia mifano kutoka katika diwani ya *Dhifa* (E. Kezilahabi) onyesha jinsi mwandishi anavyotetea maisha ya wanyonge. (alama 20)

5. Soma shairi lifuatala halafu ujibu maswali yatayofuata

MPE MTOTO HAKIYE

*Ningali kinda nishike, viungo vi teketeke
Sinipe simi nizuke, na vichaka nivifyeke
Dhibiti nivuvumke, usidiriki makeke
Pulika msikiuke, mpe mtoto hakiye*

Mungavunja haki yake, madhara milele kwake

Wa kiume na wa kike, mpeni yaliyo yake
Kwa makini mumshike, kadiri makamo yake
Pulika msikiuke, mpe mtoto hakiye.

Kwanza ni watani wake, uandae aridhike
Atuze mtima wake, maudhi yasimshike
Kuta nne zizunguke, na hofu imbandike
Pulika msikiuke, mpe mtoto hakiye.

Pili ni Chakula chake, ijengeke siha yake
Mpe titi alishike, anyonye asihinike
Husuda mbi zimwondoke, wajihii uimarike
Pulika msikiuke, mpe mtoto hakiye.

Mpe tiba 'sidhurike, ndwele asiathirike
Fikira zimpanuke, atambue rika lake
Penye daraja aruke, mvushe asighurike
Pulika msikiuke, mpe mtoto hakiye.

Angakuwa chekecheke, apande shule avuke
Mpe taaluma yake, adhibiti apanuke
Ufundi na dhima zake, ayashike ajivike
Pulika msikiuke, mpe mtoto hakiye.

Jifanye Kipenzi Chake, mpende asihinike,
Amani ijae kwake, dima asikereke,
Vizito usimtwike, visivyo vipimo vyake
Pulika msikiuke, mpe mtoto hakiye.

Elimu chuo ashike, apanuke bongo lake,
Atende jukumu lake, ahudumie wenzake,
Ajue wajibu wake, atende asitepweke
Pulike msikiuke, mpe mtoto hakiye.

Hima kwa muumba wake, muhimidi aongoke
Roho yake isafike, ahera asisumbuke
Neema imzunguke, maovu yamuepuke
Pulika msikiuke, mpe mtoto hakiye.

- a. Eleza aina ya shairi hili kwa kuzingatia i. Mishororo ii. Vina, iii. Vipande kila mshororo
iv. Mshororo wa mwisho wa kila ubeti (alama 8)
- b. Taja haki nne anazostahili mtoto (alama 4)
- c. Taja mambo mawili ambayo mtoto anahimizwa kuyatenda (alama 6)
- d. Eleza maana ya kifungu hivi; i. Pulika msikiuke ii. ningali kindi nishike (alama 2)